TAARIFA YA MATOKEO YA MITIHANI YA TAIFA YA MWAKA 2021

UTANGULIZI

Ndugu Wanafunzi, Walimu, Wazazi, Wanahabari na Wananchi kwa ujumla Assalaamu alaykum, leo tumekutana hapa kwa ajili ya kutoa Taarifa ya Matokeo ya Mitihani ya Taifa ya mwaka 2021 kama ilivyo kawaida yetu kila mwaka. Mitihani ya Taifa ya Darasa la Nne, Darasa la Sita na Kidato cha Pili hufanywa kwa lengo la kupima na hatimaye kujua kiasi cha Maarifa, Ujuzi na Muelekeo wa Wanafunzi walioupata katika kipindi chote cha kujifunza. Matokeo haya yatawasaidia Wanafunzi katika kuongeza bidii na ari ya kujifunza katika madarasa yanayofuata. Aidha mrejesho wa matokeo ya mitihani hii utawasaidia Walimu kuweza kuimarisha mbinu za kufundishia na kujifunzia kwa ajili ya kukuza uelewa wa Wanafunzi na hatimaye kuinua kiwango cha ufaulu na ubora wa elimu nchini. Matokeo ya Mitihani hii pia yatatumika katika kuwapanga wanafunzi katika ngazi ya juu kutoka ngazi aliyopo sasa.

DARASA LA NNE

UANDIKISHAJI NA MAHUDHURIO

Jumla ya watahiniwa **54,309** waliandikishwa kufanya mtihani huo katika Skuli **465** kati ya hizo **299** ni za Serikali na **166** ni za Binafsi, kati ya wanafunzi walioandikishwa Wanawake ni **26,736** sawa na asilimia **49.23** na Wanaume ni **27,573** sawa na asilimia **50.77.** Wakiwemo watahiniwa **61** wenye Mahitaji Maalumu, kati yao Wasioona ni **03**, Uoni Hafifu **17**, Viziwi **25**, Walemavu wa Viungo **03**, Walemavu wa Akili **07** na Ulemavu Mchanganyiko **06**. Idadi hii imeongezeka kwa watahiniwa **3,357** sawa na asilimia **6.18** ikilinganishwa na watahiniwa **50,952** walioandikishwa kwa

mwaka 2020. Watahiniwa **52,290** sawa na asilimia **96.28** walifanya mtihani huo ambapo wanawake ni **26,188** sawa na asilimia **50.08** na wanaume ni **26,102** sawa na asilimia **49.92.** Aidha, jumla ya watahiniwa **2,019** sawa na asilimia **3.71**hawakufanya mtihani huo kutokana na utoro na ugonjwa.

MATOKEO KWA DARASA LA NNE

Ufaulu unaonesha kuwa jumla ya watahiniwa **41,231** sawa na asilimia **78.85** wamefaulu wakiwemo wanawake **22,371** sawa na asilimia **42.78** na Wanaume **18,860** sawa na asilimia **36.07** Wanafunzi **11,059** sawa na asilimia **21.15** hawakufaulu. Aidha, watahiniwa **46** wenye Mahitaji Maalumu wamefaulu na **15** hawakufaulu. Ufaulu huu umeshuka kwa asilimia **2.55** ikilinganishwa na ufaulu wa asilimia **81.40** wa mwaka 2020. Matokeo yanaonesha kuwa ufaulu katika daraja **A**,**B**, na **C** umepanda kwa kuwa na asilimia **47.47** ikilinganishwa na asilimia **40.8** ya mwaka 2020.

UFAULU KIWILAYA

Katika Mtihani huu Wilaya ya Mjini inaongoza kwa Ufaulu wa Jumla kwa kuwa na asilimia **87.55** ikifuatiwa na Wilaya ya Kusini yenye asilimia **83.52.** Aidha, Wilaya ya Mkoani imepata asilimia ndogo ambayo ni **63.44.**

WATAHINIWA KUMI BORA KITAIFA KWA DARASA LA NNE

Mwanafunzi **Munir Ali Said** kutoka Skuli ya **Great Vision** anaongoza kwa Darasa la Nne

NAMBA YA MTAHINIWA	JINA LA MTAHINIWA	JINSI	WILAYA	JINA LA SKULI	WASTANI	NATIJA
ZP.402/0054/21	MUNIR ALI SAID	M	MAGHARIBI A	GREAT VISION SCHOOL	91	1
ZP.304/0017/21	JAMILA MBWANA MWINYI	F	MAGHARIBI B	FEZA	88.5	2
ZP.402/0050/21	MAHIR SULEIMAN KHAMIS	M	MAGHARIBI A	GREAT VISION SCHOOL	88	3
ZP.304/0028/21	RETAJ FEISAL KHAMIS	F	MAGHARIBI B	FEZA	87.5	4
ZP.411/0004/21	BIMKUBWA IDDI SEIF	F	MAGHARIBI B	EDEN INT SCHOOL	87.25	5
ZP.435/0017/21	AMINI OTHMAN JOSEPH	M	MAGHARIBI A	UPENDO NUR & PRI SCHOOL	87	6
ZP.402/0028/21	ZAHRA ALLY SHABANI	F	MAGHARIBI A	GREAT VISION SCHOOL	86.5	7
ZP.385/0025/21	NASSIR SAIDI SUFIAN	M	MAGHARIBI A	UNIQUE LEARNING 'B' BUBUBU	86.5	8
ZP.304/0007/21	ELHAN VANDEN ABEELE	F	MAGHARIBI B	FEZA	86.25	9
ZP.319/0063/21	MUHAMMAD ABUBAKAR ALI	M	MJINI	MEMON ACADEMY	85.75	10

SKULI KUMI ZILIZOFANYA VIZURI KITAIFA KWA DARASA LA NNE
SKULI ZENYE WATAHINIWA 45 NA ZAIDI

JINA LA SKULI	WILAYA	IDADI YA WATAHINIWA	WASTANI	NATIJA
FEZA	MAGHARIBI B	49	69.98	1
MADRASATUL-AHBAAB	MAGHARIBI B	55	67.4	2
GREAT VISION SCHOOL	MAGHARIBI A	65	65.36	3
FRANCIS MARIA	MAGHARIBI B	72	58.8	4
ALI KHAMIS CAMP	CHAKE CHAKE	79	58.13	5
BRIGHT FUTURE ACADEMY	MAGHARIBI B	67	58	6
BRILLIANT ACADEMY	MAGHARIBI A	129	55.92	7
GLORIOUS ACADEMY	MJINI	289	55.47	8
HIGH-VIEW SCHOOL OF ZANZIBAR	MAGHARIBI B	92	54.23	9
MEMON ACADEMY	MAGHARIBI B	77	54.02	10

SKULI KUMI ZILIZOFANYA VIZURI KITAIFA DARASA LA NNE

SKULI ZENYE WATAHINIWA CHINI YA 45

JINA LA SKULI	WILAYA	IDADI YA WATAHINIWA	WASTANI	NATIJA
WINNERS SCHOOL ACADEMY	KATI	12	72.17	1
EDEN INT. SCHOOL	MAGHARIBI B	12	71.79	2
UPENDO NUR & PRI SCHOOL	MAGHARIBI A	26	69.23	3
AL-KHAIRAT MADRASAT ISLAMIYA	MAGHARIBI A	25	66.57	4
NEW GOLDEN ACADEMY	MAGHARIBI A	15	63.22	5
LEERA SCHOOL	MAGHARIBI B	25	61.77	6
YUSSUF ENGLISH MEDIA	MAGHARIBI A	13	61.52	7
BRITISH SCHOOL	MAGHARIBI B	7	60.46	8
RAS-ISLAND ELEGANT SCHOOL	MAGHARIBI A	11	59.82	9
IKH-LAS NURSERY & PRIMARY SCHOOL	MAGHARIBI A	34	59.69	10

DARASA LA SITA

UANDIKISHAJI NA MAHUDHURIO

Uandikishaji wa watahiniwa wa Mtihani wa Taifa wa Darasa la Sita ulifanyika katika Skuli **427** kati ya Skuli hizo, Skuli **284** ni za Serikali na **143** ni za Binafsi. Kuna ongezeko la Skuli **30** sawa na asilimia **7.56** ikilinganishwa na Skuli 397zilizoandikishwa mwaka 2020.

Watahiniwa **47,469** waliandikishwa kufanya mtihani huo kati yao Wanawake ni **24,752** na asilimia **52.14** na Wanaume ni **22,717** sawa na asilimia **47.86**, wakiwemo watahiniwa **74** wenye Mahitaji Maalumu, kati yao Wasioona ni **01**, Uoni Hafifu **38**, Viziwi **17**, Walemavu wa Viungo **06**, Walemavu wa Akili **10** na Ulemavu Mchanganyiko **02**. Idadi hii imeongezeka kwa watahiniwa **13,250** sawa na asilimia **27.91** ikilinganishwa na watahiniwa **34,218** walioandikishwa mwaka 2020.

Watahiniwa **46,355** walifanya mtihani huo sawa na asilimia **97.65** ambapo wanawake ni **24,436** sawa na asilimia **52.71** na wanaume **21,920** sawa na asilimia **47.29.** Aidha watahiniwa **1,088** sawa na asilimia **2.29** hawakufanya Mtihani huo kutokana na sababu mbali mbali zikiwemo utoro na ugonjwa.

MATOKEO KWA DARASA LA SITA

Ufaulu unaonesha kuwa jumla ya watahiniwa **19,927** sawa na asilimia **42.99** kati ya **46,355** waliofanya mtihani huu wamefaulu kwa madaraja ya **A, B na C** ambao **213** watapangiwa katika madarasa ya vipawa, michepuo **2,167** na **17,547** Sekondari za kawaida.

Watahiniwa **25,752** waliofaulu kwa kiwango cha **D** wataendelea na

masomo ya darasa la saba kwa mwaka wa masomo 2022 na watahiniwa **676** sawa na asilimia **1.46** hawakufaulu. Aidha, watahiniwa **65** wenye Mahitaji Maalumu wamefaulu na **09** hawakufaulu.

Ufaulu huo umepanda kwa asilimia **0.20** ukilinganishwa na ufaulu wa asilimia **98.34** wa mwaka 2020. Aidha, Ubora wa ufaulu unaonesha kuwa idadi ya watahiniwa waliofaulu kwa daraja **A, B** na **C** umeshuka kwa asilimia **4.08** ukilinganishwa na asilimia **47.07** ya mwaka 2020.

UFAULU KIWILAYA

Katika Mtihani huu Wilaya zote zimefanya vizuri, zikiongozwa na Wilaya ya Micheweni kwa Ufaulu wa asilimia **99.74** ikifuatiwa na Wilaya ya Mkoani yenye asilimia **99.60.** Aidha, Wilaya ya Kusini imepata asilimia ndogo ambayo ni **95.61.**

WATAHINIWA KUMI BORA KITAIFA DARASA LA SITA

Mwanafunzi **Nilam Ali Mzee** wa skuli ya **Kidongo Chekundu 'A'** anaongoza kwa Darasa la Sita

NAMBARI YA MTIHANI	JINA LA MWANAFUNZI	JINSI	WILAYA	JINA LA SKULI	WASTANI	NATIJA
ZP.014/0087/21	NILAM ALI MZEE	F	MJINI	KIDONGO CHEKUNDU 'A'	87.1	1
ZP.356/0007/21	NURU SALUM WILLIAM	F	MAGHARIBI B	MADRASATUL-AHBAAB	86.86	2
ZP.003/0037/21	MEIYYA FAUZ MOHAMED	F	MJINI	DARAJANI	85.78	3
ZP.317/0063/21	YASMYNAT HUMOUD ALEY	F	MAGHARIBI B	LAUREATE SCHOOL OF ZANZIBAR	84.98	4
ZP.356/0003/21	FAT-HIYA SALUM MOHAMED	F	MAGHARIBI B	MADRASATUL-AHBAAB	84.98	5
ZP.342/0089/21	RAIYYAN SALUM JUMA	F	MJINI	GLORIOUS ACADEMY	84.28	6
ZP.018/0373/21	MAHMOUD HASSAN OMAR	M	MJINI	NYERERE	84.12	7
ZP.402/0015/21	YASINTA MARCO MAGOYI	F	Magharibi A	GREAT VISION SCHOOL	83.82	8
ZP.435/0022/21	JEMSI YUSSUPH MUSSA	M	Magharibi A	UPENDO NUR & PRI SCHOOL	83.78	9
ZP.356/0019/21	MBAROUK AMOUR KHAMIS	M	MAGHARIBI B	MADRASATUL-AHBAAB	83.62	10

SKULI KUMI ZILIZOFANYA VIZURI KITAIFA KWA DARASA LA SITA ZENYE WATAHINIWA 45 NA ZAIDI

JINA LA SKULI	WILAYA	IDADI YA WATAHINIWA	WASTANI	NATIJA
BRIGHT FUTURE ACADEMY	MAGHARIBI B	50	62.73	1
TURKISH MAARIF SCHOOL ZANZIBAR	MAGHARIBI B	94	60.15	2
HIGH-VIEW SCHOOL OF ZANZIBAR	MAGHARIBI B	62	58.76	3
TRIFONIA ACADEMY	MAGHARIBI B	80	58.09	4
GLORIOUS ACADEMY	MJINI	230	56.58	5
AL-HARAMYN INTERGRATED SCHOOL	MAGHARIBI B	123	54.19	6
MAHAD ISTIQAMA	KATI	80	53.65	7
FRANCIS MARIA	MAGHARIBI B	88	53.19	8
AMINI ISLAMIC	CHAKE CHAKE	59	52.73	9
AL-HUDAA MUSLIM SCHOOL	MAGHARIBI A	90	52.15	10

SKULI KUMI ZILIZOFANYA VIZURI KITAIFA DARASA LA SITA ZENYE WATAHINIWA CHINI YA 45

JINA LA SKULI	WILAYA	IDADI YA WANAFUNZI	WASTANI	NATIJA
MADRASATUL-AHBAAB	MAGHARIBI B	25	74.85	1
UPENDO NUR & PRI SCHOOL	MAGHARIBI A	26	68.48	2
GREAT VISION SCHOOL	MAGHARIBI A	33	68.21	3
COSMOS PRE ,PRIMARY SCHOOL	MAGHARIBI B	14	67	4
EVERGREEN SCHOOL	MAGHARIBI B	23	65.32	5
EDEN INT SCHOOL	MAGHARIBI B	11	63.25	6
FIRDAUS ISLAMIC SCHOOL	MAGHARIBI A	15	62.78	7
FEZA	MAGHARIBI B	41	62.6	8
YUSSUF ENGLISH MEDIA	MAGHARIBI A	13	62.31	9
LEERA SCHOOL	MAGHARIBI B	15	62.29	10

KIDATO CHA PILI

UANDIKISHAJI NA MAHUDHURIO

Uandikishaji wa watahiniwa wa Kidato cha Pili ulifanyika katika Skuli **295** kati ya skuli hizo, Skuli **216** ni za Serikali na **79** ni za Skuli Binafsi. Kuna ongezeko la Skuli **24** ikilinganishwa na Skuli **271** zilizoandikishwa mwaka 2020.

Jumla ya watahiniwa **32,935** walioandikishwa kufanya mtihani huo kati yao wanawake ni **17,386** sawa na asilimia **52.79** na wanaume ni **15,549** sawa na asilimia **47.21,** wakiwemo watahiniwa **75** wenye Mahitaji Maalumu, kati yao Wasioona ni **03**, Uoni Hafifu **48**, Viziwi **13**, Walemavu wa Viungo **03**, Walemavu wa Akili **7** na Ulemavu Mchanganyiko **01**. Idadi hii ni pungufu kwa watahiniwa **857** sawa na asilimia **2.60.**

MATOKEO KWA KIDATO CHA PILI

Jumla ya watahiniwa **25,227** sawa na asilimia **78.95** kati ya **31,955** waliofanya mtihani huu wamefaulu kwa madaraja ya **A, B+,B, C** na **D** na watahiniwa **6,728** sawa na asilimia **21.05** hawakufaulu. Aidha, watahiniwa **57** wenye Mahitaji Maalumu wamefaulu na **18** hawakufaulu.

Ufaulu huo umepanda kwa asilimia **0.28** ikilinganishwa na ufaulu wa asilimia **78.67** wa mwaka 2020. Kwa ujumla ufaulu wa daraja **A,B+ na B** umepanda kwa asilimia **14.25** ukilinganisha na **12.96** wa mwaka 2020. Watahiniwa **25,227** wataendelea na masomo ya Kidato cha Tatu na watahiniwa **6,728** watarudia Kidato cha Pili kwa mwaka wa masomo 2022.

UFAULU KIWILAYA

Wilaya zote zimefanya vizuri ambapo Wilaya ya Micheweni inaongoza kwa kupata ufaulu wa Jumla wa asilimia **86.31** na Wilaya ya Kusini imepata asilimia ndogo ya **53.89.**

WATAHINIWA KUMI BORA KITAIFA KIDATO CHA PILI

Mwanafunzi **Shaib Hamad Shaib** wa Skuli ya Sekondari ya **Fidel Castro** anaongoza kwa Kidato cha Pili.

NAMBARI YA MTIHANI	JINA LA MWANAFUNZI	JINSI	WILAYA	JINA LA SKULI	WASTANI	NATIJA
ZS.189/0051/21	SHAIB HAMAD SHAIB	M	CHAKE CHAKE	FIDELCASTRO	88.04	1
ZS.189/0014/21	NAFHAT HAMAD SALIM	F	CHAKE CHAKE	FIDELCASTRO	85.64	2
ZS.189/0050/21	SAMIR ABASS JUMA	M	CHAKE CHAKE	FIDELCASTRO	85.46	3
ZS.019/0087/21	HASNU MOHAMMED HAJI	M	MJINI	LUMUMBA	84.56	4
ZS.189/0035/21	HASSAN HAMAD FAKI	M	CHAKE CHAKE	FIDELCASTRO	84.54	5
ZS.189/0030/21	ABDULSAMAD ALI KHALFAN	M	CHAKE CHAKE	FIDELCASTRO	84.39	6
ZS.337/0025/21	MAKAME SAID KHAMIS	M	MAGHA RIBI B	LEERA SCHOOL	84.07	7
ZS.189/0034/21	HAMED OMAR AHMED	M	CHAKE CHAKE	FIDELCASTRO	83.6	8
ZS.189/0042/21	NASSOR HAMAD ABDALLA	M	CHAKE CHAKE	FIDELCASTRO	83.57	9
ZS.189/0041/21	NASSOR ABEID SABIRI	M	CHAKE CHAKE	FIDELCASTRO	83.49	10

SKULI KUMI ZILIZOFANYA VIZURI KITAIFA KWA CHA KIDATO CHA PILI ZENYE WATAHINIWA 45 NA ZAIDI

JINA LA SKULI	WILAYA	IDADI YA WATAHINIWA	WASTANI	NATIJA
FIDELCASTRO	CHAKE CHAKE	56	76.44	1
LUMUMBA	MJINI	111	68.15	2
MADUNGU 'B'	CHAKE CHAKE	80	63.23	3
MIKINDANI DOLE	MAGHARIBI 'A'	106	60.06	4
CCK KIUYU	MICHEWENI	52	59.74	5
FEZA	MAGHARIBI 'B'	46	58.26	6
TUMEKUJA	MJINI	111	57.11	7
UTAANI 'B'	WETE	45	55.26	8
HIGH-VIEW SCHOOL OF ZANZIBAR	MAGHARIBI 'B'	77	55.08	9
MAHAD ISTIQAMA	KATI	69	54.97	10

SKULI KUMI ZILIZOFANYA VIZURI KITAIFA KIDATO CHA PILI ZENYE WATAHINIWA CHINI YA 45

JINA LA SKULI	WILAYA	IDADI YA WATAHINIWA	WASTANI	NATIJA
MADRASATUL AHBAB	MAGHARIBI B	17	67.65	1
LEERA SCHOOL	MAGHARIBI B	31	66.63	2
KENGEJA UFUNDI	MKOANI	44	54.72	3
BRILLIANT ACADEMY	MAGHARIBI B	42	53.01	4
AL-MARFAA ISLAMIC SCHOOL	MAGHARIBI A	25	52.56	5
MADUNGU 'A'	CHAKE CHAKE	37	51.84	6
EDEN INT SCHOOL	MAGHARIBI B	7	51.63	7
BRIGHT FUTURE ACADEMY	MAGHARIBI B	22	51.37	8
PHILTER FEDERAL	MAGHARIBI B	20	51.34	9
SKY VIEW SECONDARY SCHOOL	MAGHARIBI B	18	49.95	10

KESI ZA UDANGANYIFU

Katika Mitihani ya Mwaka 2021 hakukuwa na kesi yoyote ya udanganyifu kwa Darasa la Nne, Sita na Kidato cha Pili.

PONGEZI ZA WIZARA

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa dhati kabisa inawapongeza wanafunzi wote waliofaulu katika mitihani yao kwa kuweza kuendelea na masomo katika madarasa yanayofuata na wanaombwa kuongeza bidii ili waweze kukuza uwezo wao wa kitaaluma kwa ajili ya kupata ufaulu mzuri zaidi katika mitihani ijayo.

Aidha, Wizara inatoa pongezi kwa Walimu kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuwapatia wanafunzi taaluma na maadili mema mambo ambayo yatawasaidia wakati wa sasa na baadae.

Pia Wizara inaendelea kuwashukuru Wazazi na walezi wa wanafunzi kwa kuwasimamia, kuwalea, kuwaongoza na kuwapatia watoto wao huduma za lazima ili waweze kumudu masomo yao.

Aidha, Wizara inatoa shukurani kwa wale wote walioshiriki katika kufanikisha ufanyaji wa mitihani hii katika hatua zake zote.

KUANGALIA MATOKEO.

Ndugu wanafunzi, Walimu na Wananchi kwa ujumla, Wizara inapenda kuwaarifu kwamba matokeo ya mitihani hii yanaonekana katika tovuti zifuatazo:-

www.moez.go.tz na www.bmz.go.tz

Ahsanteni kwa kunisikiliza.

ALI KHAMIS JUMA
KATIBU MKUU
WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI
ZANZIBAR.